

Title: Under the Mango Trees

EPISODE 6

Author: Romie Singh

Editors: Susanne Fuchs, Katrin Ogunsade, Maja Braun

List of characters for episode 6:

- Narrator
- Desirée
- Endurance
- Lorraine
- Alice
- Eric
- April
- Bongo
- Children in background

INTRO

Hujambo na karibu kwenye sehemu ya sita ya Noa Bongo Jenga maisha Yako mchezo ulioandikwa na Romie Singh kwa jina Chini Ya Miembe. Mchezo huu wa kulisimua unaangazia kwa kina maswala ya familia hususan mpango wa Uzazi na njia tofauti za kupanga uzazi. Leo hii kijana Eric anavinjari namna ya kumkaribia zaidi rafiki mpendwa wa dada yake pacha, Desirée. Endurance, afurahishwa na mchezo wanaocheza na rafiki zake shuleni. Desirée nae atarajia kupata habari ambazo hakuzitegemeai kwa mengi zaidi jiunge nasi!

SIG.TUNE UP HOLD UNDER AND FADE

NARRATOR: Desirée alikuwa bado anatetemeka. Bongo, ajenti wa muziki, alikuwa amempigia simu muda mchache uliopita kumuelezea habari nzuri lakini simu ikakatika. Hivi sasa Desirée anaisubiri simu ya Bongo kwa hamu kubwa. Wakati huo huo, nduguye Endurance, alionekana kuwa na hamu ya kutaka kuzungumza. Siku hizi amekuwa ni mwenye furaha tele.

Sc. 1 Interior

1. **SFX:** children playing in the background
2. **ENDURANCE:** Wajua. Tunafurahia sana kucheza vitu hivi vya plastiki wakati wa mapumziko. Huwa tunavijaza maji halafu tunawamwagia wasichana!
3. **DESIRÉE:** (distant) Vitu vya plastiki?
4. **ENDURANCE:** (laughing) Basi acha kuingalia simu yako wakati wote! Unajua ninamaanisha nini Des.
5. **DESIRÉE:** wala sielewi, – ni Maputo au nini?

6. ENDURANCE: (giggling) hapana, wacha ujinga! Ni Kondomu!
Huwa tunazijaza maji Kondomu halafu
tunawakimbiza wasichana! Lakini
tafadhali usimwambie nyanya!
7. DESIRÉE: Hata siwezi. Lakini hizo plastiki. Hebu
niambie huwa mnapazita wapi hizo
Kondomu?
8. ENDURANCE: Huwa tunaziokota katika vyoo vya
wanaume katika mikahawa ya mji wa
Kentown.
9. DESIRÉE : (laughing) Endurance! Natumai kuwa unajua kazi
yake, mbali na kuwa nyinyi mnazigeuza
kuwa ni mabomu ya maji!
10. ENDURANCE: Najua bwana. Bi.Davies kila mara huwa
anzungumzia juu ya Kondomu wakati
akizungumzia kuhusu HIV na magonjwa
ya zinaa wakati wa somo la maisha
darasani.
11. DESIRÉE: Na unajua kuzitumia barabara, sina shaka.
12. ENDURANCE: (moaning) Oh dada wee, Tafadhali
usinifedheheshe!

13. DESIRÉE: Sawa! Hebu jifanye kuwa wewe ndio Bi.Davies na mimi ni mwanafunzi. Enhe utaniambia nini?
14. ENDURANCE: (Mimicking teacher's voice) Wewe, Desirée, wewe msichana mkorofi! Kaa vizuri!
15. DESIRÉE: Wacha utani, Endurance! Zungumza kama mwalimu! Jaribu kunieleza!
16. ENDURANCE: (clears throat) Sawa. Kondoms bora zimetengenezwa kwa latex. Unamvisha mwanaume Kondom kwenye um... er... unajua ni kitu gani, halafu itakapokuwa mahala pake sawasawa, basi inamzuia msichana kupata mimba na pia inamkinga msichana na mvulana kutokana na maambukizi ya virusi vya HIV au magonjwa ya zinaa. Oh ndio, na unahitajika kutumia Kondomu mpya kila mara. Pia ni lazima uangalie muda wake wa kumalizika matumizi ! Chunga usiitoboe kwa kucha zako. Sawa? Maelezo yamekwendaje?
17. DESIRÉE: (clapping) Mmh, umeacha maelezo mengi tu, lakini vizuri! Nakupa alama saba kwa kumi!

18. **ENDURANCE:** Mimi, nimejifunza mengi kutoka kwa marafiki zangu, haswa wavulana wakubwa zangu kiumri . Bi. Davies huwa anakatisha mazungumzo pale yanapo anza kunoga!
19. **SFX** Phone rings
20. **DESIRÉE:** (excited) Sawa, Endurance. Hii ni simu muhimu sana. Huyu ni Bongo anapiga tena. Naitambua namba yake, kwa hivyo nakuomba utoke ili nipate kuzungunza nae kwa utulivu.
21. **ENDURANCE:** (cheerfully) Sawa. Nitakuwa mtoto mzuri! (sticking tongue out). Errrr
22. **DESIRÉE:** (big sigh, then speaking louder) Hallo? Oh, habari Bongo!
23. **BONGO:** Samahani simu ilikatika wakati ule, Vipi uko peke yako ? twaweza kuzungumza?
24. **DESIRÉE:** Naam. Hakuna wasiwasi. Ninakusikiliza.
25. **BONGO:** Sawa. Mac ni ajenti mwingine wa muziki katika mji wa Granville tena mashuhuri kuliko mimi. Alisikiliza sauti yako niliyo inasa na (with emphasis) ali... yaani

ali... bloo.... anasema kuwa wewe ndie unayefaa kwenda kwenye mashindano na sio Lorraine. Sauti unayo!

26. DESIRÉE: Mimi? Hata siamini!
27. BONGO: Ndio hivyo, biashara ya muziki wa Pop ndivyo ilivyo! Tunataka ushiriki katika muda wa wiki tatu zijazo... Desirée? Upo?
28. DESIRÉE: Bongo. siwezi! Lorraine ni rafiki yangu mpendwa . Siwezi kumfanyia hivyo. Anatarajia kuchaguliwa , sio mimi.
29. BONGO: Sikiliza, ni vigumu kuhusu Lorraine siwezi kuwashirikisha nyinyi nyote. Kwa hivyo ni mmoja wenu tu aliye na nafasi wewe au yeye. Ama uingie kivyako bila usaidizi wangu.
30. DESIRÉE: Nadhani hunielewi. Mimi nina jukumu la kuwatunza watoto watano. Hakuna mtu mwingine na wala mimi siwezi kuwatelekeza. Halafu kuna swala la usafiri. Mimi siwezi kugharimia...
31. BONGO: (strictly) Nakuuliza unataka kuwa mwimbaji au hutaki. Usinipotezee muda , Des, kipaji

chako. Na nafasi hii ni ya mara moja maishani.

32. DESIRÉE: lakini siwezi ni... ni nje ya upeo wangu.

33. BONGO: Je hilo ni jibu lako la mwisho?

34. DESIRÉE: (long pause) Yes, Bongo.

35. BONGO: (Frustrated sigh) Oh, jamani! Huu si wazimu huu. Tazama iwapo utataka kuzungumza tena kuhusu jambo lolote nibipu halafu mimi nitakupigia. Huwezi kuiachia nafasi kama hii ikupite, Des. Kama nilivyo kwambia usimwambie Lorraine chochote. Mimi nitaongea nae. Natumai hii hatakuwa buriani, Des.

36. DESIRÉE: breaks into tears.

NARRATOR: Desirée alibubujikwa na machozi! Lo ni mtihani gani huo katika maisha yake, hali iliyokaribia kabisa kutimiza ndoto yake ya kuwa mwanamuziki. Je ataipata tena nafasi kama hiyo? Kilomita ishirini mbali na yeye, Lorraine alikuwa akisubiri kwa shauku kubwa mlio wa simu. Na ilipolia haikuwa yake.

Scene 3 Interior

37. **SFX:** General dinner time noises - plates, cutlery, stirring food etc.
38. **SFX:** Phone ringing
39. **LORRAINE:** (Scraping chair) (off mic) Hallo? (disappointed)
Oh, sawa nitamuita yes. (whispering)
Mama? niyako!
40. **ALICE:** (off mic; loudly) Hallo? Oh, hallo! naam... hapana...
ndio... vizuri sana! Vyema hakuna neno.
Watafurahi sana! Sawa sawa.
Tutazungumza kwa kina kesho.
Nashukuru kwa kunifahamisha Thank you .
Kwaheri.
41. **ERIC:** (chewing food) Habari nzuri?
42. **LORRAINE:** Tafadhali, simu! haraka, mama!
43. **ALICE:** (happy) Ndio! Habari nzuri sana. Alikuwa ofisa mkuu wa afya. Hatimae! Huduma ya afya ya jamii itakuwepo Mtelera! Amesema huduma hiyo itanza rasmi katika kipindi cha miezi miwili. Halafu ameniambia kuwa wamenichagua mimi kuwa ndio msimamizi mkuu wa kliniki!

44. ERIC: Wow! Hiyo ni habari nzuri sana! Kwa hiyo utapanda cheo kutoka kuwa daktari hadi meneja, kama baba .
45. ALICE: (Stirring spoon in pot) Isipokuwa. (tasting food)
Hmmm, umepika mchuzi mtamu sana, Eric. Unajua, tuna ardhi katika kijiji cha Mtelera, ambayo tuliirithi kutoka kwa mababu zetu, na nyumba pia.
46. ERIC: (Shocked) Eti tuna nyumba? Mtelera?
47. ALICE: Ndio! Mimi na baba yako tumekuwa tukizungumzia kuhusu kwenda kuishi shamba baada ya kustaafu. Kwa hivyo naweza nikaifanyia matengenezo nyumba ile halafu nikaishi wakati nikifanya kazi.
48. ERIC: (forcing himself to sound calm) Ni sawa. vizuri. Viazi vimeiva sasa, Ma.

NARRATOR: mara tu aliposikia kuhusu nyumba ya familia iliyopo Mtelera, Mpango ulianza kujengeka kichwani mwa Eric. Lakini alitaka kuupa nafasi mpango huo ujengeke vyema taratibu. Huu haukuwa wakati muafaka wa kufanya maamuzi. Lorraine alikuwa akihangaika huku na huku akiomba moyoni mwake Bongo apige simu na atoe habari nzuri alizokuwa akizitarajia. Hatimae, simu ililia!

Scene 4 Interior

49. **SFX:** Phone ringing
50. **LORRAINE:** (very excited) Naam?
51. **BONGO:** Lorraine?
52. **LORRAINE:** Naam, Bongo? Nimesubiri sana simu yakol. Niambie, je Mac alipenda?
53. **BONGO:** zaidi ya hayo. Alibloo kweli kweli. Umefaulu. Vipi uko tayari?
54. **LORRAINE:** Bila shaka! na Des?
55. **BONGO:** Hamna! Hana ulichonacho. Wewe ndio sauti, Lorrie!
56. **LORRAINE:** Oh, wow! Lakini namsikitikia. Alifanya vizuri sana.
57. **BONGO:** Sasa, nakutaka uje ofisini kabla ijumaa ili uje utie saini mkataba, nina imani kubwa na wewe!

NARRATOR: Kwa hivyo, Lorraine hakujua kuwa rafikiye Desirée haswa ndie aliyekuwa amechaguliwa badala yake. Wakati Lorraine alipokuwa anapaa mawinguni kwa furaha, Desirée aliwaza iwapo atapata nafasi nyingine kama ile ili atimize nia yake kwanza ya kuwa mwanamuziki.

58. **SFX:** Wind in the trees up, evening ambiance

NARRATOR: Alipokuwa anatembea kwenye msitu wa miembe Desirée alihisi kuwapo kwa wahenga wa familia yake, alihisi uwepo wa kina baba, kina mama na watoto waliotangulia mbele za haki. Mawazoni mwake alihisi anawapa mawazo yake huku upepo ulipokuwa unapepea polepole mitini. Alisikia sauti ya mama yake ikinong'ona nyuma yake.

59. **APRIL:** (with echo) Usiwe mnyonge. Uamuzi wako ulikuwa sawa.

60. **DESIRÉE:** Alaa nimefanya sawa? Nina majonzi makubwa, Mama. Lakini pia nina faraja. Wao walifikiri kuwa mimi ndie bora! Hilo tu linamaana! Labda nitakuwa mwanamuziki! Lakini nitaweza kweli kutia mkazo katika shughuli za kuimba mimi?

61. **APRIL:** (with echo) Watoto ni wadogo sana kuishi peke yao, na nduguyo Endurance pia anakuhitaji. Anaendelea kuimarika kutokana na

mapenzi na malezi yako. Anaendelea kukua vizuri sana.

62. DESIRÉE: Nafahamu. Na mimi nampenda pia tena sana, Mama! Lakini ndugu yangu anamtamani sana baba. Baba ametupotea. Yuko mahali katika mji wa Granville lakini sijui ni wapi haswa. Mama, Eric ni mkarimu sana.

63. APRIL: (echo) Eric ni mkarimu.

64. DESIRÉE: Amesema atanisaidia kumtafuta baba.

65. APRIL: (with echo) Mtafute baba. Masikini Babu. Nenda ukamtafute yeye ni baba yako. Oh, hebu niimbie mwanangu! Utapata nafasi nyingine tena! Wewe bado ni mtoto. Niimbie kwa sauti yako nzuri.

66. DESIRÉE: Sings signature tune

OUTRO.

Ni hayo tu kwa leo katika Noa Bongo Jenga Maisha Yako. Mchezo wa kulisimua unaoangazia umuhimu wa kupanga uzazi na jinsi mpango huo unavyoweza kujenga familia yenye furaha. Kupanga uzazi kunawapa wanawake pamoja na wandani wao fursa ya kuchagua wakati muafaka wa kupata watoto. Nakualika ujiunge nasi kwenye

sehemu ya saba wakati ambapo Eric apata mawazo mapya jinsi ya kumkaribia zaidi Desirée na matarajio ya Lorraine ya kuwa pop idol yaanza kuyumba yumba.

Unaweza kuusikiliza tena mchezo huu na kumbuka kumwambia rafiki yako ausikilize pia. Anuani yetu ya mtandao n: d w world dot d e mkwaju l b e

Kwaheri hadi wakati mwingine tutakapo kutana tena.

END OF EPISODE SIX